Je, watoto wetu wanajifunza? Jarida la Uwezo Tanzania

# TUZUNGUMZE ELIMU

Mei 2021 Toleo No. 001




*Mwanafunzi wa shahada ya Uzamivu akizungumza wakati wa warsha.*

## Wasomi wa Chuo Kikuu wahamasika kutumia takwimu za Uwezo


Zaida ya wanafunzi 25 wa shahada ya Uzamivu katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es salaam(DUCE) wameeleza matakwa yao ya kutaka kutumia takwimu za tathmini za Uwezo za kupima ujifunzaji wa watoto, wakati wanapoandika tafiti zao na machapisho mengine.

Hayo yalisemwa na wanafunzi wenyewe wakati walipotembelea ofisi za Uwezo Tanzania na kushiriki katika semina ya elimu iliyoandaliwa na Shirika hilo na kwa kushirikiana na wakufunzi wa Chuo hicho na kufanyika tarehe 02 Machi 2021.

Aidha katika warsha hiyo Uwezo iliwasilisha kwa wanafunzi wa DUCE ripoti ya tathmini ya Uwezo ya mwaka 2019, ambayo ilionesha takwimu za viwango halisi vya ujifunzaji na umahiri walio nao watoto wa miaka 6-16 katika kusoma na kufanya hesabu. Pia uwezo walieleza uzoefu wao katika kufanya jitihada za Uwezo na Jamii pamoja na Jifunze ambazo zimekuwa msaada mkubwa kwa kusaidia kuinua stadi za kusoma na hisabati kwa watoto nchini.

Alinukuliwa mwanafunzi mmoja akizungumza wakati wa warsha hiyo alisema, hii ni miongoni mwa warsha nzuri ambazo miongoni mwa alizohudhuria. “Takwimu za Uwezo ni nzuri sana hasa unapozitumia kufanya uchambuzi wa sera ya Elimu pamoja na matokeo ya Ufundishaji kwa watoto. Tutashukuru sana kama mtaturuhusu tuwer tunazitumia katika kuandaa tafiti zetu na maandiko mengine ya kielimu”.

# Tovuti ya UwezoTanzania Yazinduliwa




Shirika la UwezoTanzania hivi karibuni limefanikiwa kuzindua tofuti yake mpya www.uwezotanzania.or.tz ambayo inatarajiwa kuwa nyenzo muhimu ya kuendeleza mawasiliano na wadau mbalimbali ili kuwasilisha kazi zake na pia mafanikio yaliyofikiwa katika kazi hizo.

Uwezo pia imekuwa ikifanya vizuri katika mtandao wa twitter @UwezoTanzania ambapo imefanikiwa kufuatwa na zaidi ya watu mia tano ndani ya muda mfupi.

Kupitia tovuti ya Uwezo, utaweza kujipatia taarifa mbalimbali ikiwemo miradi yote Uwezo wanayotekeloeza hyivi sasa na pia mafanikio makubwa yaliyofikiwa tangu kuanzishwa kwa jitihada ya Uwezo nchini Tanzania mwaka 2009, Chini ya Shirika la Twaweza.

“Hii ni nyezo muhimu sana ya mawasiliano ambayo tulikuwa tunaisubiria kwa muda sasa, tulihitaji hii kuwa miongoni mwa tovuti bora, kwa kweli tuna jivunia kuwa nayo sasa. Watu wote mnakaribishwa kuitembelea na kupata taarifa muhimu mnazozihitaji”. Alinukuliwa akizungumzia tovuti hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Uwezo Tanzania, Zaida Mgalla.

# Serikali yaipongeza uwezo kwa kuleta jitihada ya Jifunze

SERIKALI wilayani kilolo Mkoani Iringa imelipongeza Shirika la UwezoTanzania kwa kuja na mradi wa siku 30, wa kufundisha wanafunzi wanaoshindwa kumudu stadi muhimu za kusoma na kufanya hesabu.


Naibu Mkuu Mdhibiti Ubora wa Shule, Wilaya ya KILOLO, Beatrice Komba alimwambia mwandishi wa habari wa E FM radio **Rachel Chacha** wakati alipotembelea wilayani humo hivi karibuni kuwa analipongeza shirika la UwezoTanzania kwa kuwa wabunifu na kuja na hii mbinu muhimu ya ufundishaji ya jifunze ambayo kwa muda mfupi imesaidia watoto wengi kumudu stadi muhimu za kusoma na kuandika.

Komba alisema, mradi huo umeweza kuonesha mafanikio makubwa kuhakikisha kuwa kila mtoto anayeenda shule anaweza kumudu stadi muhimu za kusoma na kufanya hesabu rahisi.

Amesema serikali wilayani humo imezipenda mbinu za ufundishaji zinazotumiwa na uwezo Tanzania katika darasa la lifunze, kwani zimelenga siyo tu kuwezesha wanafunzi kujua kusoma na kufanya hesabu bali kuliwezesha taifa kuwa na wahitimu wa elimu ya msingi wenye uwezo wa kusoma na kufanya hesabu rahisi.



*Walimu kutoka Wilaya za Kilolo, Ludewa na Mbarali wakiwa katika mafunzo ya Jifunze hisabati yaliyofanyika Mapema mwaka huu Mjini Makambako*




# TaRL Africa yatoa mafunzo kwa mashirika yanayotekeleza mbinu ya TaRL

Shirika maarufu barani Africa linalotekeleza mbinu ya Teaching at the Right Level(TaRL), hivi karibuni liliandaa mafunzo kwa wadau mbalimbali barani humo ambao wanajihusisha na kutelekeleza mbinu ya TaRL na kuwasaidia watoto wajifunze.

Mafunzo hayo yaliyofanywa kwa njia ya mtandao, yalihudhuriwa na washiriki toka nchi mbalimbali barani Africa zikiwemo Nigeria, Botswana, Tanzania, Uganda, na Kenya .

Ambapo, mfanyakazi wa shirika la UwezoTanzania, Benjamin Masebo ni miongoni mwa washiriki waliohudhuria mafunzo ya Shirika la hayo ambayo yalifanyika kwa muda wa wiki moja hivi karibuni.

Akiwasilisha mbele ya wafanyakazi wengine wa Uwezo juu ya nini amejifunza, masebo alisema mafunzo hayo yalikuwa mazuri sana na kwa hakika amepata mbinu mpya nyingi za kuwasaidia watoto kujifunza ujuzi muhimu katika hisabati na kusoma.

Aidha, alisema atahakikisha anazitumia mbinu hizo kuwafundisha walimu wengine wengi ili waweze kuwasaidia watoto wengi nchini kujifunza.

Shirika la UwezoTanzania ni mwanzilishi wa Mbinu ya Teching at the right level nchini Tanzania, tangu lilipoanza utekelezaji wa mbinu hii hapo mwaka 2019, Mbinu hii imesaidia watoto wengi waliokuwa wakishindwa kumudu stadi muhimu za kusoma na kufanya hisabati. Ili kufahamu zaidi kuhusu shirika la TaRL Africa tembelea tovuti yao :- https://www.teachingattherightlevel.org/

KUTOKA KWA MASHIRIKA WADAU WA UWEZO

# SAWA yaendesha mafunzo ya TaRL Shule ya Msingi Leena

Mapema mwezi Aprili mwaka 2021, Sawa Wanawake Tanzania(SAWA), zamani ilijulikana kama "Safina Women's Association" (SAWA) waliendesha mafunzo ya mbinu ya Teaching at the Right Level(TaRL) kwa walimu wa Shule ya Msingi na Chekechea ya Leena iliyopo Manipaa ya Morogoro Mkoani Morogoro.

Shule hiyo inayomilikiwa na shirika la SAWA ilianzishwa kwa lengo la kuwa shule ya mfano katika kutoa Elimu Jumuishi katika uwanja wa elimu ndani ya mkoa huo, ambapo ili kufikia lengo hili, SAWA imeweka juhudi zake katika kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu ili kuwawezesha watoto wote wakiwemo wale ktutoka mazingira magumu na wenye mahitaji maalum wapate elimu iliyobora.

Leena inawachukulia watoto ambao wameacha kujifunza kutoka kiwango fulani cha kujifunza kuwa wana mahitaji maalum ya kujifunza. Watoto hawa hawana ujuzi wa msingi wa kujifunza. SAWA imetumia Ufundishaji katika ngazi aliyofikia mtoto ambao imejifunza kutoka UWEZO Tanzania na ambao wameanza kutekeleza tangu mwaka 2019 katika wilaya za Kisarawe, Mvomero na Chamwino.

Mbinu ya TaRL ambayo Shirika la SAWA wameanza kuitekeleza sasa imethibitishwa kuwa imefanya kazi na kuleta matokeo makubwa sana katika maeneo mengi ya ulimwengu kwa kuwasidia watoto kujifunza stadi muhimu za hisabati na kusoma.


Shirika la SAWA limekuwa mdau na Mshirika wa Muda mrefu sana wa UWEZO Tanzania ambapo wamekuwa wakishirikiana kufanya tathmini za Uwezo za watoto kujifunza tangu mwaka 2010.



*Wafanyakazi wa shule ya Leena wakifanya mazoezi ya TaRL*

## JE? WAJUA

### Wasichana wengi wanashindwa kuendelea na masomo kwasababu ya Mimba?




*Chanzo: Mwananchi data.*

**Waandishi :**
Greyson Mgoi
&
Benjamin Masebo
**Wahariri**
Greyson Mgoi
Zaida Mgalla
**Kwa maoni wasiliana na mhariri kwa anuani:-**
Uwezo Tanzania
S.L.P. 8259 Kinondoni,
Dar es salaam, Tanzania
**Mitandao ya Kijamii**
Twitter: @UwezoTanzania
**Barua pepe**:
info@uwezotanzania.or.tz
**Tovuti:**
www.uwezotanzania.or.tz

## KUTOKA MAGAZETINI

HABARI

### Rais Samia ataka maboresho ya Elimu nchini

Hivi karibuni, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Samia Suluhu alinukuliwa akisema kuwa anaitaka wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuangalia upya mfumo wa elimu ambao utakuwa na manufaa kwa wanafunzi na ambao utamwandaa mwanafunzi kujitegemea. Rais Samia aliitaka wizara hiyo kuangalia namna bora ya kutoa elimu pamoja na kuangalia mitaala ya elimu na kuiboresha. Chanzo: https://habarileo.co.tz/habari/2021-04-06



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh.Samia Suluhu*